**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA WA MGONJWA DUNIANI**

Dodoma, Septemba 17, 2025

Tarehe 17 Septemba kila mwaka, Tanzania inaungana na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kuadhimisha Siku ya Usalama wa Mgonjwa Duniani.

Siku hii muhimu huadhimishwa na WHO kwa kushirikiana na wanachamawa Shirika hilo kwa lengo la kuongeza uelewa, kushirikisha jamii, na kuhamasisha hatua za pamoja ili kuimarisha usalama wa mgonjwa katika ngazi zote za utoaji huduma za afya.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni ***'Huduma Salama kwa kila Mtoto Mchanga na kila Mtoto'*** ikiwa na ujumbe mahususi wa ***'Usalama wa Mgonjwa Tangu Anapozaliwa'***. Kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha jitihada za pamoja za kuhakikisha watoto wachanga na watoto kwa ujumla wanapata huduma za afya zilizo salama, zenye ubora na zinazozuia madhara yanayoweza kuzuilika.

Serikali inaendelea na juhudi za kuboresha huduma za watoto na watoto wachanga (Neonatal Care Unit – NCU) ambapo Wodi Maalum za Watoto Wachanga zimeongezeka kutoka wodi 14 mwaka 2018 hadi 362 kufikia Juni 2025.

Pamoja na hayo Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuimarisha huduma za watoto wachanga ikiwemo upatikanaji wa vifaa na vifaa tiba, kuwajengea uwezo watoa huduma zaidi ya 8000 kwa mwaka 2025 kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuhamasisha vituo vyote kuanzisha NCU katika ngazi zote kulingana na miongozo.

Vilevile Wizara inaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma za afya ili kuhakikisha viwango vya ubora na usalama vinafuatwa na kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii, wazazi na walezi katika kulinda haki za wagonjwa na watoto wachanga ikiwemo kupata huduma salama.

Imetolewa na;

Dkt. Grace Magembe

**MGANGA MKUU WA SERIKALI**